

Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 katika kuboresha mchakato huu kulikuwa na awamu ya pili ya kutangaza zabuni mwezi wa Agosti.

10. Swali; Ni maboresho gani ambayo Wakala umeyafanya katika kuboresha huduma zake katika kipindi cha awamu ya tano?

Jibu; Wakala umeboresho sehemu ya ugomboaji na uondoshaji mizigo kwa kuongeza rasilimaliwatu na vitendea kazi ambapo taasisi zote za umma zinazotumia huduma hii zinapata kwa wakati.

Wakala umeongeza muda wa kutoa huduma ya mafuta kwa ajili ya magari ya serikali ambapo sasa huduma hiyo inapatikana nchi nzima kuanzia saa moja na nusu(1.30) asubuhi mpaka saa kumi na mbili jioni (12.00) siku zote za wiki ikiwemo na sikukuu za kitaifa. Pia Wakala unazidi kusogea huduma zake wilayani ambapo GPSA mkoa wa Shinyanga umeongeza ofisi ndogo katika wilaya ya Kahama ambayo imeanza kazi Februari, 2019.

Na.	Kifungu cha Sheria/Kanuni	Jukumu Linaloendana na Kifungu cha Kanuni husika
i.	Kifungu 44; kanuni 77	Kununua kwa niaba ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuvi wa Umma(PPRA) na Mamlaka ya Rufaa ya Zabuni za Umma(PPAA), vifaa na huduma mbalimbali.
ii.	Kifungu 43; Kanuni 46(c)	Kununua vifaa na huduma kwa niaba ya Taasisi za Umma.
iii.	Kifungu 50; Kanuni 131	Kuanda utaratibu wa ununuvi wa vifaa na huduma mtambuka kwa kutumia mikataba maalum.
iv.	Kifungu 56; Kanuni 130,135	<ul style="list-style-type: none">● Kuuza vifaa na huduma kwa taasisi za Umma● Kununua vifaa na mafuta moja kwa moja kutoka kwa watengenezaji.
v.	Kanuni 130(5)	Kutoa huduma ya ugomboaji na uondoshaji wa mizigo kwa taasisi za umma.
vii.	Kanuni 134	Kutoza tozo ya huduma za ununuvi kwa PPRA, PPAA.

11. Swali; Wakala unaongozwa na sheria zipi katika utekelezaji wa majukumu yake?

Jibu; Sheria ya Ununuvi wa Umma, 2011 ikisomwa na marekebisho yake ya mwaka 2016 na kanuni za ununuvi wa umma zimeipa GPSA majukumu kuititia vifungu na kanuni zifuatazo:

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:-

Mtendaji Mkuu

Wakala wa Huduma ya Ununuvi Serikalini (GPSA)

Mtaa wa Bohari na Barabara ya Nyerere,

Eneo la Keko Mwanga,

SLP 9150,

Dar es Salaam

Simu: +255 22 286 6071/286 1617

Nukushi: +255 22 286 6072

Tovuti: www.gpsa.go.tz

Barua pepe: ceo@gpsa.go.tz

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

**WAKALA WA HUDUMA YA
UNUNUVI SERIKALINI**



**MASWALI YANAYOULIZWA
MARA KWA MARA**

UTANGULIZI

Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa kwa mujibu wa sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 ya mwaka 1997 na kutangazwa kwenye gazeti la Serikali Na. 235 la tarehe 7 Desemba, 2007. Aidha Agizo la uanzishwaji lilifanyiwa mabadiliko tarehe 13 Aprili, 2012 kupitia Tangazo Na.133. Wakala ulizinduliwa rasmi tarehe 16 Juni, 2008 na una ofisi katika Makao Makuu ya Mikoa yote ya Tanzania Bara.

1. Swali: GPSA inasaidiaje kupunguza gharama za ununuzi Serikalini?

Jibu: Kupitia ununuzi wa pamoja wa vifaa na huduma mtambuka (VHM) unaofanywa na GPSA, gharama za mchakato wa zabuni zinapungua kwa kiasi kikubwa sana kwa kuzingatia idadi ya taasisi za umma ambazo zinatumia fedha za umma, kama kila moja ingeendesa mchakato wa zabuni wa kununua vifaa na huduma wanazohitaji gharama kwa Serikali ingekuwa kubwa sana.

2. Swali: Taasisi za umma zinanufaika vipi na huduma zinazotolewa na GPSA?

Jibu: Taasisi za umma hupata vifaa na huduma kwa haraka, kwa gharama nafuu, na vyenye ubora unaolingana na thamani ya fedha. Ununuzi kupitia GPSA hauna urasimu na taasisi hazianzishi mchakato wa zabuni kwa vifaa na huduma zinazopatikana GPSA.

3. Swali: Ni kwa namna gani wafanyabiashara na makam-puni binafsi yananufaika na huduma za GPSA?

Jibu: GPSA hununua vifaa na huduma kutoka kwa wafanyabiashara kwa njia ya uwazi na ushindani, hivyo fursa sawa hutolewa kwa wafanyabiashara wote. Aidha kupitia ununuzi wa pamoja wa vifaa na huduma mtambuka, wafanyabiashara wanapata taarifa zote za zabuni na kushiriki kwenye zabuni kupitia taasisi moja tu badala ya kwenda kwenye kila taasisi. Utaratibu huu unawapunguzia wafanyabiashara gharama na muda wa kuzunguka kwenye taasisi. Aidha ni rahisi kwa wafanyabiashara kupata oda moja kwa moja kutoka kwenye taasisi ununuzi bila kulazimika kushindanishwa upya.

4. Swali: Utaratibu gani unatumika kwa wafanyabiashara kuingia kwenye orodha ya wazabuni wa kuuza vifaa na huduma mtambuka (VHM) katika taasisi za umma?

Jibu: GPSA hutangaza zabuni kila mwaka ifikapo mwezi Februari ambapo wafanyabiashara wenye nia ya kufanya biashara na Serikali wanatakiwa kuomba zabuni na kuzingatia masharti ya zabuni. Baada ya uchambuzi wa maombi ya zabuni, wale walioitimiza masharti hupewa mikataba na kuwekwa kwenye orodha ya wazabuni wa kuuza vifaa na huduma mtambuka (VHM) kwa taasisi zote za serikali. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 GPSA iliboresha utaratibu huu kwa kutangaza tena zabuni kwa mara ya pili mwezi Agosti ili kutoa fursa kwa walokosa na waombaji wapya na zoezi hili litaendelea kufanyika mara mbili kila mwaka.

5. Swali; Ni kwa nini GPSA hulipwa kwanza kabla ya kutoa huduma/vifaa tofauti na wazabuni wengine ambao hutoa huduma/vifaa na kisha kulipwa?

Jibu: Hii ni kwa sababu GPSA sio mzabuni, hufanya ununuzi kwa niaba ya serikali na hivyo utaratibu wa malipo ni tofauti na ule unaooneshwa kwenye kanuni za ununuzi.

6. Swali: Inakuwaje taasisi nunuzi zinatangaza zabuni za vifaa na huduma ambazo zinatangazwa na GPSA na hatua gani zinachukuliwa kudhibiti hali hiyo?

Jibu: Kwa mujibu wa sheria ya ununuzi wa umma, ununuzi wa vifaa na huduma mtambuka unatakiwa kufanyika kupitia utaratibu unaoandaliwa na GPSA. Kwa sababu hiyo taasisi yoyote ya umma inayotangaza na kuendesha mchakato wa zabuni wa vifaa na huduma mtambuka inakwenda kinyume na matakwa ya sheria kifungu Na. 50, kanuni ya 131. PPRA ndio wenye mamlaka ya kusimamia sheria na taratibu za ununuzi wa umma kama itathibitika kuvunjwa kwa sheria hiyo na taasisi husika.

7. Swali: Ni utaratibu gani hutumika kupata vifaa na huduma kutoka GPSA?

Jibu: Vifaa na huduma zinazopatikana kutoka GPSA zimeord-heshwa katika “stores catalogue” ambayo inapatikana katika tovuti ya GPSA: www.gpsa.go.tz na pia kwenye chapisho linalotolewa na GPSA. Taasisi inapohitaji kifaa au huduma iliyoored-heshwa katika chapisho hilo inatakiwa kuanda agizo la mahitaji hayo kupitia kwenye fomu (CRIN) ambayo hujazwa na kuwasilishwa GPSA kwa ajili ya kuandaliwa Ankara. Baada ya Ankara kufanyiwa malipo, taasisi hupatiwa mara moja vifaa husika.

8. Swali: Kuna tofauti gani kati ya majukumu ya GPSA na PPRA?

Jibu: GPSA ni Wakala wa Serikali ambao majukumu yake ni kutoa huduma za ununuzi wa vifaa na huduma mtambuka katika Serikali. PPRA ni Mamlaka ya udhibiti wa ununuzi wa Umma ambayo husimamia utekelezaji wa sheria ya ununuzi wa Umma na kujenga uwezo wa taasisi za Umma katika ununuzi.

9. Swali: Ni wakati gani zabuni za ununuzi wa vifaa na huduma mtambuka hutangazwa na Wakala?

Jibu: Zabuni za ununuzi wa vifaa na huduma mtambuka hutangazwa kila mwaka kati ya mwezi Februari na Machi. Mchakato huo hufanyika hadi kufikia wiki ya kwanza ya mwezi Juni ambapo matokeo hutolewa kupitia t ovuti ya Wakala: www.gpsa.go.tz. Matokeo huambatana na kusudio la Afisa Masuuli la kutoa tuzo kwa walioshinda zabuni pamoja na orodha ya wazabuni walioshindwa pamoja na sababu za kushindwa kwao. Katika kipindi hicho ambacho hudumu kwa muda wa siku saba, mzabuni anaweza kutuma malalamiko yoyote kwa Mtendaji Mkuu kuhusiana na mchakato wa zabuni.